JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ina utaratibu wa kutoa taarifa ya utendaji wa Sekta ya Mawasiliano kila robo mwaka kupitia tovuti ya Mamlaka www.tcra.go.tz. Dhumuni la taarifa hii kwa vyombo vya habari ni kutoa mukhtasari kuhusu maendeleo ya sekta ya mawasiliano kwa robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023.

***Kuhusu huduma za simu***

Ripoti hii ya utendaji wa kisekta imeonesha ongezeko la asilimia 3.4 kwa laini za simu zinazotumika, ambapo hadi mwezi Juni 2022 kulikuwa na laini Milioni 56.2 idadi iliyoongezeka hadi kufikia laini milioni 58.1 Septemba 2022. Idadi hii ya laini za simu inahusisha line zinazotumiwa na watu na laini zinazotumiwa kwa ajili ya mawasiliano kati ya mashine kwa mashine (M2M)

Aidha, takwimu zinaonyesha kwamba mikoa mitano (5) Tanzania inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya laini za simu zinazotumika yaani (Active SIM-cards) hadi Septemba 2022 ni:- Dar es salaam (Laini Milioni 9,756,697), Mwanza (Laini 3,700,914), Arusha (3,448,200), Mbeya (3,089,848), na Tabora (3,060,407).

Uchambuzi wa laini hizo kwa watoa huduma unaonyesha kwamba kuna ushindani mkubwa; kwani hakuna mtoa huduma mwenye zaidi ya asilimia 35 ya laini zilizosajiliwa.

Mwelekeo wa usajili kwa miaka mitano iliyopita unaonyesha ongezeko la asilimia nane (8) kwa mwaka. Kuenea kwa laini miongoni mwa watu kumeongezeka kwa asilimia nne (4) kwa mwaka. Kuenea kulikuwa asilimia 78 mwaka 2017, asilimia 81 mwaka 2018, asilimia 88 mwaka 2020 na asilimia 91 mwaka 2021.

***Kuhusu gharama za vifurushi vya simu na data***

Wastani wa gharama za vifurushi vya simu zilikuwa shilingi 7.8 kwa kupiga simu ndani ya mtandao mwezi Septemba 2022, kutoka shilingi 7.7 Juni 2022. Pamoja na ongezeko hili dogo, gharama bado ni chini kulinganisha na vifurushi vya simu kwenda mitandao mingine. Wastani wa vifurushi vya simu kwenda mitandao mingine ulikuwa shilingi 8.1 Septemba 2022; ikiwa ni ongezeko kutoka shilingi 7.6 Juni 2022.

Wastani wa gharama za data Septemba 2022 zimebakia kuwa shilingi 1.8 (kwa MB) kama ilivyokuwa Juni 2022.

Mawasiliano Towers, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Fax: +255 22 2412009-10
Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz
ISO 9001:2015 Certified

***Idadi ya watumiaji wa huduma za intaneti***


Watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka 29,169,958 Juni 2022 hadi 31,122,163 Septemba 2022 sawa na ongezeko la asilimia 6.7%

Mwelekeo wa ongezeko la watumiaji wa intaneti linaonesha kwamba kulikuwa na ukuaji wa takriban asilimia 17 kila mwaka, katika kipindi cha miaka 5 ambapo mwaka 2017, kulikuwa na watumiaji Milioni 16,106,636 na mwishoni mwa mwaka 2021 waliongezeka kufikia Milioni 29,103,482.

Matumizi ya intaneti yameongezeka kutoka wastani wa MB 6,037, kwa mtumiaji Machi 2022 hadi MB 6,626 kwa mtumiaji Septemba 2022.

***Idadi ya Watumiaji wa Mitandao ya Kijamii***

Takwimu za ripoti hii ya utendaji wa sekta ya Mawasiliano nchini zinabainisha mitandao mitano (5) ya kijamii inayotumiwa zaidi, hivyo kuongoza kwa kiwango kikubwa cha data iliyotumika kwa kipimo cha GB; ambapo Mtandao wa kijamii wa FaceBook uliongoza kwa kurekodi (GB Bilioni 2.59), ukifuatiwa na YouTube wenye (GB Bilioni 1.91), kisha WhatsApp uliokuwa na (Bilioni 1.58), na TikTok ukiwa na (GB Milioni 999) ikifuatiwa na mitandao mingine.




Uchambuzi umeonyesha Mitandao mitano ya kijamii iliyofikiwa zaidi kupitia kifaa kimojakimoja cha mtumiaji (simu, kompyuta mpakato, kiskwambi, kompyuta ya mezani). Mitandao hiyo ni kama ifuatavyo:- Facebook (Vifaa Milioni 3,487,393), WhatsApp (Vifaa Milioni 3,415,917), YouTube (Vifaa Milioni 2,846,839), Instagram (Vifaa Milioni 2610,509), TikTok (Vifaa Milioni 1,601,392).

***Kuhusu Sekta ya Utangazaji***

Takwimu za utangazaji zinaonyesha kwamba visimbuzi 3,326,845 vilikuwa hewani Septemba 2022 vikiongezeka kutoka milioni 3,169,231 Juni 2022. Kati ya hivyo, 1,656,460 ni vya dijitali kwa mfumo wa televisheni wa utangazaji wa mitambo ya ardhini (DTT) kulinganisha na 1,670,385 kwa mfumo wa televisheni kwa satelaiti.


Dar Es slaam inaongoza kwa kuwa na visimbuzi (1,270,755), ikifuatiwa na Arusha (272,702), Mwanza (261,237) na Mbeya (218,007). Mikoa yenye visimbuzi vichache ni Songwe (1,568) ukifuatiwa na Katavi (16,990).

Televisheni za waya (cable tv) zimeenea kutoka watu 16,786 waliounganishwa 2018 hadi 41,092 Septemba 2022. Huduma ya televisheni kwa waya (yaani cable Tv) imeenea mikoa ya Ziwa; ambapo mkoa wa Simiyu unaongoza; ukiwa na jumla ya waliounganishwa 4,584, ikifuatiwa na Mwanza, yenye 3,480.

***Huduma za Kifedha katika Mtandao wa simu***

Tanzania inazidi kuendeleza mfumo jumuishi wa kifedha kutokana na kuongezeka kwa watumiaji wanaofanya miamala kupitia simu za mkononi.

Takwimu za mawasiliano za mwezi Septemba 2022 zinaonyesha kwamba huduma za pesa kupitia simu za mkononi zimeongezeka. Akaunti za pesa kwa simu za mkononi zineongezeka kutoka 38,008,482 Juni 2022 hadi 39,590,502 Septemba 2022.




Idadi ya miamala imeongezeka kutoka Bil. 349,952,830 hadi miamala Bil. 366,178,409 Septemba 2022.

Akaunti za pesa kwa simu zimeongezeka kwa asilimia 1.5 katika miezi tisa iliyopita; kuanzia Januari hadi Septemba 2022; wakati miamala ikiongezeka kwa asilimia 2.

| Mwezi | Mwaka | Idadi ya Watumiaji | Idadi ya Miamala | Thamani ya Miamala |
|---|---|---|---|---|
| **JANUARI** | 2022 | 35,201,960 | 308,569,751 | 10,350,248,535,456 |
| **FEBRUARI** | 2022 | 35,578,052 | 292,626,474 | 9,539,172,477,200 |
| **MACHI** | 2022 | 35,749,298 | 330,148,997 | 10,703,041,422,029 |
| **APRILI** | 2022 | 36,068,839 | 327,324,035 | 10,321,267,168,688 |
| **MEI** | 2022 | 36,302,884 | 352,362,035 | 10,689,193,723,704 |
| **JUNI** | 2022 | 37,407,233 | 343,639,879 | 11,608,009,683,538 |
| **JULAI** | 2022 | 38,008,482 | 349,952,830 | 12,548,569,958,747 |
| **AGOSTI** | 2022 | 38,504,971 | 356,790,863 | 12,741,158,372,863 |
| **SEPTEMBA** | 2022 | 39,590,502 | 366,178,409 | 12,722,059,888,707 |

***Kuhusu huduma za Posta***

Huduma za utumaji na upokeaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi zinazidi kushamiri na kuchochea ukuaji wa biashara mtandao ambapo kwa robo mwaka ya kwanza ya 2022 vifurushi vilivyotumwa ni 513,080. Katika Sekta hii ya Posta pia tumetuma kwenda nje ya nchi jumla ya vifurushi na vipeto 49,286 na kupokea 21,962 huduma hii inaendelea kuchagiza ukuaji wa biashara mtandao au e-commerce.

***Hitimisho***

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuhakikisha Watoa Huduma wanaendelea kutoa huduma kwa ufanisi, weledi na ubora ili kukidhi mahitaji ya jamiii yetu kwa Maendeleo chanya ya uchumi wa Kidijitali.

**IMETOLEWA NA**
**MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
**25-10-2022**

Mawasiliano Towers, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Fax: +255 22 2412009-10
Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz
ISO 9001:2015 Certified